Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2008 Certified

**Ghorofa ya 7, Jengo la LAPF Pension Fund, Mkabala na Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama**
**S.L.P. 72175, Dar es Salaam, Tanzania**
**Simu: +255-022 2923513-18; Nukushi: +255-22 2923519**
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http://www.ewura.go.tz

## TAARIFA KWA WAOMBAJI WA LESENI ZA UMEME
## *(ELECTRICITY LICENCES APPLICANTS)*

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inawatangazia waombaji wote wa leseni za ukandarasi wa umeme (*electrical installation licences*), leseni za uzalishaji umeme (electricity generation licences), na leseni za usambazaji umeme (electricity distribution licences) kwamba kuanzia tarehe 1/8/2017, waombaji wote wanaohitaji kufanya maombi ya leseni hizo watume maombi yao kwa njia ya mtandao, kwa kutumia mfumo unaoitwa *Licensing and Order Information System* (LOIS) ulioanzishwa na EWURA kwa kupitia ***https://lois.ewura.go.tz***

Lengo la kutumia njia ya mtandao kutuma maombi ya leseni ni kupunguza muda wa upatikanaji wa leseni hizo zinazotolewa na EWURA, pia kuwawezesha waombaji kupata taarifa za maombi yao moja kwa moja katika mfumo huo, hivyo kuongeza uwazi.

Kwa maelezo zaidi unaweza kutembelea ofisi zetu za Makao Makuu jijini Dar es Salaam na ofisi zetu za Kanda zilizoko Arusha, Mbeya, Dodoma na Mwanza au tuma baruapepe kupitia info@ewura.go.tz au tembelea tovuti ya EWURA http://www.ewura.go.tz

**Mha. Godwin Samwel**

**KAIMU MKURUGENZI MKUU**

**EWURA**